

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA THELATHINI**

**18 MEI, 2021**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA THELATHINI – TAREHE 18 MEI, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**



Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

III. MASWALI:

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**253. MHESHIMIWA NANCY HASSAN  
NYALUSI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi,  
Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi na kuanza kutumia Hospitali ya Wilaya ya Mufindi.

**254. MHESHIMIWA SOPHIA HEBRON MWAKAGENDA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Barabara ya Kiloba – Njugilo yenye urefu wa Kilometa 7 itajengwa ili kurahisisha mawasiliano ya Wananchi na Wanafunzi wanaokwenda Kata ya Masukulu – Rungwe.

**255. MHESHIMIWA AYSHAROSE NDOGHOLI MATTEMBE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza barabara za Singida Kaskazini zinazounganisha Vijiji ambazo hazipitiki kwa sasa.

**256. MHESHIMIWA STANLAUS SHING'OMA MABULA (NYAMAGANA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itakuwa tayari kuanza Mradi wa TACTIC ili kufikia Malengo Makuu ya Serikali ya Mwaka 2020 – 2025 katika kuboresha miundombinu ya barabara.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**257. MHESHIMIWA EDWARD KISAU OLELEKAITA (KITETO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza bei na kuongeza muda wa mkopo wa Matrekta waliokopeshwa Wakulima wa Jimbo la Kiteto na Shirika la NDC.

**258. MHESHIMIWA NEEMA WILLIAM MGAYA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, ni lini Serikali itaanza kutekeleza Mradi wa Liganga na Mchuchuma ili uweze kuchangia katika kukuza Uchumi wa Taifa.



**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO  
YA MAKAZI:**

**259. MHESHIMIWA ISSA JUMANNE MTEMVU  
(KIBAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi,  
Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, ni lini Serikali itatoa Hati katika Mradi wa  
Urasimishaji kwa Wananchi wa Kata za  
Kibamba, Kwembe, Mbezi, Msigani, Goba  
na Saranga.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**260. MHESHIMIWA NDAISABA GEORGE  
RUHORO (NGARA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi  
na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Kivuko katika  
Mto Ruvuvu ili kuunganisha Vijiji vya  
Mayenzi na Kanyinya vilivyopo Wilayani  
Ngara.

**WIZARA YA MAJI**

**261. MHESHIMIWA OMARI MOHAMED KIGUA  
(KILINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itanza mkakati wa kusambaza maji kutoka Mto Dibuluma Kata ya Kibati Wilayani Mvomero kwenda katika Kata za Tunguli, Kwekivu, Masagalu na Songe Wilayani Kilindi.

**WIZARA YA KILIMO:**

**262. MHESHIMIWA INNOCENT SEBBA  
BILAKWATE (KYERWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa Wakulima wa Kahawa ndani ya muda mfupi pale wanapomaliza kupima Kahawa zao kwenye AMCOS.

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**DODOMA  
18 MEI, 2021**

**S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE**